**TAARIFA YA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (e-GA) MHANDISI BENEDICT NDOMBA, KWA MHE. BALOZI DKT. MOSES KUSILUKA KATIBU MKUU KIONGOZI, WAKATI WA UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA SITA (6) CHA SERIKALI MTANDAO TAREHE 17 FEBRUARI, 2026 KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA.**

**Mhe. Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka*;*** Katibu Mkuu Kiongozi

**Ndg. Mululi Mahendeka;** Katibu Mkuu Ikulu

**Makatibu Wakuu wote,**

**Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya,**

***Dkt. Mussa Kisaka;*** *Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Wakurugenzi*** *wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,*

***Wakuu wa Idara*** *za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali*

***Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo*** *na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao;*

**Viongozi wa Dini,**

**Waandishi wa Habari**,

*Itifaki imezingatiwa;*

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

**Kazi na Utu;**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa kibali cha uhai na uzima, na kutuwezesha kukutana hapa leo, katika Kikao Kazi hiki cha Sita (6) cha Serikali Mtandao.

Kipekee napenda kukushukuru **Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka Katibu Mkuu Kiongozi,** kwa kukubali na kuitikia wito wetu wa kushiriki nasi, katika ufunguzi wa Kikao Kazi hiki cha Sita (6) cha Serikali Mtandao. Karibu sana!

**Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;**

Kikao hiki kimehudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwemo Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Taasisi za Umma na binafsi, Watumishi wa sekta ya umma na binafsi, Viongozi wa dini, pamoja na Waandishi wa Habari. Wote wamejitokeza kuunga mkono utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

Kwa niaba ya Menejimenti na watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), tunawashukuru washiriki wote na tunathamini uwepo wenu. Tunawakaribisha na tunasema asanteni sana kwa kuja.

Kipekee, napenda kuushukuru uongozi wa Mkoa wa Arusha, kwa kutupokea na kutuwezesha kuandaa Kikao Kazi hiki kitakachofanyika kwa muda wa siku tatu kuanzia leo hii hapa jijini Arusha.

Kwa dhati kabisa naomba niwashukuru wadhamini wote **44** wa Kikao Kazi hiki cha 6 cha Serikali Mtandao, ambao kwa pamoja wamewezesha kufanikiwa kwa kikao hiki. Aidha, naomba kuwatambua wadhamini wakuu **Kumi (10)** wa Kikao Kazi hiki, ambao ni; **Kampuni ya Yas Mix by Yas, SOFTNET, INFO GEAR, Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Wizara ya Habari na Mawasiliano, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Shirika la Mendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Kampuni ya Simu za Mkononi VODACOM, Bodi ya Sukari (Sugar board), na Benki ya NMB.**

**Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;**

Kikao kazi hiki cha siku tatu, kinawakutanisha takriban wadau **1,300** wa Serikali Mtandao. **Mada 14** zinazohusu Serikali Mtandao zitawasilishwa na washiriki watapata nafasi ya kujadiliana kuhusu utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, ikiwemo kuainisha changamoto na namna ya kukabiliana nazo. Aidha, washiriki watapata taarifa ya utekelezaji wa maazimio yaliyotolewa katika kikao kazi cha tano cha Serikali Mtandao kilichofanyika mwezi Februari mwaka jana (2025), sambamba na kuweka maazimio ya kikao kazi hiki cha leo.

**Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;**

Kaulimbiu ya Kikao Kazi hiki ni "***Kuboresha Utendaji wa Serikali kwa Kuimarisha Utoaji wa Huduma za Umma Kupitia Mifumo Salama na Jumuishi ya Serikali Mtandao"***

***"Transforming government operations by enhancing public service delivery through integrated and secure e-government solutions"***

Kaulimbiu hii ina akisi dhamira ya Serikali ya kutumia mifumo ya kidijitali iliyo salama na jumuishi ili kuongeza ufanisi, tija, uwazi na uwajibikaji katika utendaji kazi, pamoja na kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi.

**Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;**

Mamlaka imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao, kwa kuhakikisha matumizi ya TEHAMA Serikalini yanakuwa salama na shirikishi, na kuzingatia viwango na miongozo ya Serikali Mtandao, ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2019.

Hadi sasa, Mamlaka imefanikiwa kuimarisha usimamizi wa miradi ya TEHAMA Serikalini, usimamizi na uendeshaji wa Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Government Network - GOVNET), pamoja na uoni wa jumla (end to end visibility ) wa mifumo ya TEHAMA ya Serikali na mingine inayotoa huduma Serikalini. Hatua hii imechangia kupunguza urudufu wa mifumo, kuimarisha ubadilishanaji wa taarifa Serikalini baina ya mifumo ya taasisi

mbalimbali pamoja na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za umma kwa kutumia TEHAMA. Hii ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050 kupitia lengo la kuhakikisha, zaidi ya asilimia 80 ya huduma za serikali zinapatikana kupitia mifumo ya kidijitali iliyo salama na jumuishi ifikapo mwaka 2050. Pia ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2025 Ibara ya 46 ambayo, pamoja na mambo mengine inaelekeza huduma za Serikali asilimia 50 zipatikane kupitia mifumo ya kidigitali ifikapo 2030.

Pia, Mamlaka imeendelea kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa Vituo Vya Serikali Vya Kuhifadhi Data (Government Data Centers), ambavyo vimewezesha taasisi nyingi za Serikali kuhifadhi na kuendesha mifumo yao kwa usalama, ufanisi na uhakika wa upatikanaji wa huduma kwa wakati wote. Hatua hii imeongeza usalama wa taarifa za Serikali na kupunguza gharama za uendeshaji wa miundombinu ya TEHAMA.

Vilevilea, Mamlaka imefanikiwa kuimarisha uwezo wa taasisi za umma kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao kupitia mafunzo, usimamizi na ushauri wa kitaalamu, jambo ambalo limeongeza ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa miradi ya TEHAMA katika taasisi za umma.

Aidha, Mamlaka inaendelea kutumia jukwaa hili muhimu la kikao kazi kusikiliza changamoto za utekelezaji wa miradi ya TEHAMA Serikalini, kubadilishana uzoefu, na kuweka mikakati ya pamoja itakayohakikisha ajenda ya mageuzi ya kidijitali Serikalini inatekelezwa kwa mafanikio makubwa zaidi.

**Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;**

Mamlaka kupitia Kituo chake cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGovernment Research, Innovation and Development Centre - eGOVRIDC), hufanya tafiti na bunifu mbalimbali za huduma za serikali mtandao kwa ajili ya kutatua changamoto zilizopo, ikiwemo kuboresha utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa umma kwa wananchi.

Katika utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao, Mamlaka hushirikiana na sekta za umma na binafsi, zikiwemo benki, kampuni za simu na watoa huduma mbalimbali wa vifaa na miundombinu ya TEHAMA. Kikao hiki ni moja ya ishara ya ushirikiano tulionao.

**Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;**

Nitumie fursa hii kumshukuru **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, kwa jitihada zake za kuwekeza katika sekta ya TEHAMA na mageuzi ya kidijitali Serikalini, sambamba nakuiwezesha Mamlaka kutekeleza majukumu yake ikiwemo, ujenzi wa Mfumo unaowezesha Mifumo ya Serikali Kuwasiliana na Kubadilishana taarifa, ujulikanao kama ***Government Enterprises Service Bus*** **(GovESB).** Ubadilishanaji wa taarifa kupitia mfumo huu, umechochea kuongezeka kwa ufanisi wa utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa wananchi.

**Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;**

Utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao katika taasisi za umma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao umeongeza umahiri na ufanisi mkubwa wa kiutendaji, ikiwemo katika kuanzisha, kuendesha na kusimamia miradi ya TEHAMA. Hali hii imeifanya nchi yetu kutambuliwa kimataifa katika kupiga hatua za maendeleo ya Serikali Mtandao. Mafanikio haya ni pamoja na:-

- Tuzo ya Umoja wa Mataifa ya Ubunifu katika Huduma za Umma kwa mwaka 2024 *'**UN Public Service Innovation Awards, 2024'*** kupitia mfumo wa e-Mrejesho.

- Tuzo ya Umoja wa Mataifa ya '**World Summit on the Information Society -WSIS 2025'** katika kipengele cha Serikali Mtandao kupitia mfumo wa eMrejesho toleo la pili (eMrejeshoV2).

- Ripoti ya U*komavu wa Matumizi ya Teknolojia Duniani katika Utoaji wa Huduma za Serikali na Ushirikishwaji wa Wananchi* **- GovTech Maturity Index (GTMI)** ya Benki ya Dunia mwaka 2025, ambapo Tanzania imeorodheshwa katika **Kundi A - Ukomavu wa Juu wa Kuenea Zaidi kwa Matumizi ya TEHAMA (Extensive GovTech Maturity).** Hii ni mara ya pili kwa Tanzania kutambuliwa na Benki ya Dunia (WB) katika kupiga hatua ya Ukomavu wa TEHAMA, ambapo mwaka **2022** Tanzania ilitajwa kuwa miongoni mwa nchi zilizofanya vizuri zaidi duniani na kushika Nafasi ya Pili Afrika. .

**Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;**

Pamoja na mafanikio haya tuliyonayo, bado kuna changamoto kadhaa zinazopunguza ufanisi wa utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao. Baadhi ya changamoto hizo ni uhaba wa wataalamu wabobezi wa TEHAMA katika maeneo mbalimbali na kasi kubwa ya mabadiliko ya teknolojia yanayotokea duniani na kuhitaji Maafisa TEHAMA kujengewa uwezo mara kwa mara ili kukabiliana na mabadiliko hayo.

Changamoto nyingine ni kutofanyika kwa vikao vya Kamati za TEHAMA za taasisi *'ICT Institutional Steering Committee'* kwa wakati kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Serikali Mtandao, ambapo athari yake ni kuwepo kwa mifumo ya TEHAMA ndani ya Taasisi ambayo haijibu mahitaji ya Idara zote husika ndani ya Taasisi, hivyo kutokuwa na tija iliyokusudiwa..

**Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;**

Baada ya kusema haya, napenda kukushukuru na kukukaribisha tena katika Mkutano huu wa sita (6) wa Serikali Mtandao.

Asanteni sana kwa kunisikiliza,

***"Kwa pamoja tuijenge Serikali Mtandao"***